TANGAZO LA SERIKALI NA. 463 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7 na 13)*

## SHERIA NDOGO YA USHURU WA LANGO LA LODUARE YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Lango la Loduare ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro ya mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria hii itatumika katika eneo la lango la Loduare (Hifadhi ya Ngorongoro)

Tafsiri

3. Katika Sheria hii isipokuwa pale Muktadha utahitaji vinginevyo
"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro.

Wajibu wa magari kulipa ushuru

4. Kila gari la utalii, mabasi na malori ambayo yatapita katika lango la Loduare lililowekwa na Halmashauri yatalipa ushuru kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria hii.

Ushuru kwa watalii wa Tanzania na watalii wa Kigeni

5. Kila mtalii atakayeingia kapitia lango la Loduare atatozwa ushuru kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili ya Sheria hii:

Makosa

6. Mtu yoyote atakayekiuka masharti ya Sheria ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatiaatatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua Shilingi laki mbili na kisichozidi Shilingi Milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

*Tangazo La Serikali Na. 463 (Linaendelea)*

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4)*

| Namba | Aina ya Gari | Kiasi cha Ushuru | |
|---|---|---|---|
| | | (Shilingi) | USD |
| 1. | Gari dogo la utalii mpaka uzito wa kg 2000 lenye usajili wa Tanzania. | 2,000.00 | - |
| | Gari dogo la utalii mpaka uzito wa kg 2000 lenye usajili wa nje ya Tanzania | - | 20 |
| 2. | lori au basi lenye uzito zaidi ya kg 2000, lenye usajili wa Tanzania | 50,000.00 | - |
| | lori au basi yenye uzito zaidi ya kg 2000 lenye usajili wa nje ya Tanzania | - | 30 |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya Aya ya 5 (a) na (b))*

| Namba | Uraia | Kiasi cha Ushuru | |
|---|---|---|---|
| | | (Shilingi) | USD |
| 1. | Watu wazima ambao siyo raia wa Tanzania | - | 15 |
| 2. | Mtu mzima mtanzania | 1,500.00 | |
| 3. | Mtoto chini ya miaka 16 ambao siyo raia wa Tanzania | - | 5 |
| 4. | Mtoto chini ya miaka 16 raia wa Tanzania | 500.00 | - |

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio la mkutano wa Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro ulioitishwa na kufanyika tarehe 10 September, 2023 mbele ya:-

NASSORO B. SHEMZIGWA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro*

MOHHAMED F. BAYO
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
30 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*